KAZI ZA MKUU WA MKOA.

Mkuu wa Mkoa alifanya ziara katika Halmashauri zote

Na, Afisa habari wa mkoa, Humphrey kisika.

tano(5) Halmashauri ya Iringa dc, Kilolo dc, Mufindi dc, Mafinga mji na Manispaa ya Iringa.

Kwa kipindi cha Octoba – Disemba, 2018 Mkuu wa Mkoa ameendelea na kazi zake kama ifuatavyo:-

Ulinzi na Usalama

Mhe.Mkuu wa Mkoa katika kuimarisha ulinzi na usalama aliwataka wazazi, walezi, Viongozi wa dini na vyombo vya ulinzi na usalama kukemea vitendo vya ubakaji na mimba kwa wanafunzi na Watoto wadogo ambavyo kwa sasa matukio hayo yapo kwa kiasi kikubwa.

Uhifadhi na Utalii

Mkuu wa Mkoa alihimiza wananchi na wadau kushiriki kwenye maonesho ya utalii yaliyofanyika kuanzia tarehe 12/12/2018 hadi 16/12/2018 kwenye viwanja vya kichangani. Aidha, aliwataka wadau wa utalii kuendelea kuwekeza kwenye sekta ya utalii hususani ujenzi wa mahoteli makubwa na kumbi za mikutano.

Uchumi na Biashara

Mkuu wa Mkoa alikagua Viwanda katika Wilaya ya Mufindi ambapo aliwataka wafanyakazi wa viwanda hivyo kufanya kazi kwa kujituma. Aidha, aliwataka wamiliki wa viwanda kuwathamini wafanyakazi katika viwanda hivyo na kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu. Wakuu wa Wilaya waliagizwa kutoa msaada pindi changamoto mbalimbali zinapojitokeza kwenye viwanda.

Mkuu wa Mkoa alifanya uzinduzi rasmi wa ugawaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo ambapo alikabidhi vitambulisho 5000 kwa kila Halmashauri.

Afya

Mkuu wa Mkoa aliongoza kikao cha lishe kilichofanyika tarehe 12/11/2018. Katika kikao hicho alihimiza kuwa Lishe iwe agenda ya kudumu kwa kuwa

hali ya lishe kwa mkoa wa Iringa sio nzuri hivyo hamasa iendelee kutolewa kwa wananchi.

Aidha, alihimiza kuendelea na usafi wa mazingiza hususani wananchi kuwa na vyoo bora ili kupunguza magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Alikutana na mashirika yote yasiyo ya kiserikali na kuwataka kuendelea kutoa michango yao kwenye mapambano dhidi ya HIV na lishe. Aidha, aliwataka kila mwezi kuwasilisha taarifa za shughuli wanazotekeleza katika maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa alitoa msimamo wa Serikali ya Mkoa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa juu ya eneo la ujenzi wa Hospitali ya wilaya kutokana na mvutano uliokuwepo ambapo alielekeza Hospitali ijengwe eneo la Igodikafu badala ya Ihemi kwa kuwa Ihemi iko jirani na hospitali kubwa ya Mkoa, Hospitali ya Mafinga, Kilolo na Ipamba, ambapo alisisitiza kuwa maamuzi hayo yamezingatia maslahi mapana ya wananchi wa maeneo ya pawaga ambao wako mbali na huduma za Afya ukilinganisha na maeneo mengine , ubovu wa miundombinu ya barabara na magonjwa ya mlipuko yanayotokea mara kwa mara. Msimamo huo wa Serikali ya Mkoa umezingatia pia mapendekezo ya taarifa za timu maalumu za wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

Elimu

Mkuu wa Mkoa alikagua na kujiridhisha na usalama wa Mitihani ya kidato cha NNe na Cha pili katika mkoa wa Iringa.

Aidha, alikuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya Chuo Kikuu RUCU yaliyofanyia tarehe 17/11/2018. Katika mahafali hayo, aliwataka wahitimu elimu waliyoipata iwasaidie kujiajiri na kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mazingira yao.

Mkuu wa Mkoa alitembelea shule ya Nyang’oro na kuwashukuru wafadhili kwa kuwajengea hosteli ya wanafunzi wa kike shuleni hapo.

Serikali za Mitaa

Mkuu wa Mkoa aliongoza kikao cha kujadili hoja za Mkaguzi wa Ndani kwa Halmashauri zote. Alielekeza kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wasiende likizo mpaka hoja hizo ziwe zimefungwa.

Kilimo.

Mkuu wa Mkoa aliwataka wakulima kutumia mbolea kwa wakati. Aidha, aliwataka maafisa kilimo kutoa taarifa sahihi ya upatikanaji wa mbolea na masoko kwa wakulima ili iwe rahisi kupata huduma.

Mkuu wa Mkoa alihimiza kuwa suala la Mbolea lipewe kipaumbelea hasa kwa maafisa kilimo kuwasaidia wakulima kuwapa elimu ya pembejeo na kufuatilia upatikanaji wa mbolea kwa wakati.

Miundombinu

Mkuu wa Mkoa alifanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya barabara za TARURA na TANROADS wilaya ya Kilolo na Mufindi. Wakati wa Ukaguzi wa barabara hizo aliwataka wakandarasi kukamilisha kazi hizo kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyotolewa na kwa wakati ili kuharakisha maendeleo kwa wananchi.

Aidha, alizindua na kukagua miradi ya umeme wa TANESCO na REA na kuwataka wananchi kutunza miundombinu ya miradi hiyo ya umeme.

Mkuu wa Mkoa alikutana na Viongozi wa Bodaboda, bajaji na daladala pamoja na SUMATRA, RTO na manispaa na kuwawataka kumaliza tofauti na changamoto zinazowakabili kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo za usalama barabarani.

Usafiri wa Anga

Mkuu wa Mkoa alihimiza ukarabati wa kiwanja cha Ndege nduli (Run way) na pia jengo la kusubiria abiria vikamilishwe kwa wakati na kwa kuzingatia ubora. Aidha alikutana na viongozi wa Mamlaka za Usafiri wa Anga na kukubaliana kuwa ifikapo Machi, 2019 ndege kubwa zianze kufika Iringa.

Michezo

Alikutana na viongozi wa timu ya Lipuli na kuwataka kuachana na makundi na badala yake kuwa wamoja ili kuhakikisha wanapata ushindi kama timu moja. Aidha, aliwataka kuwa na mikakati ya kutafuta fedha za uendeshaji wa timu ikiwa ni pamoja na kupata wadhamini. Mkuu wa Mkoa aliwaahidi kuwa patafanyika kikao cha wadau wote wa michezo ili kupata maoni ya wadau.

Mkuu wa mkoa aliwapatia Tsh 1,000,000/= kwa ajili ya kuwasapoti wachezaji wa Lipuli, ili kuamsha morali na kuleta ushindi.